الدُّعَاءُ الَّذِيْ لَا يُرَدُّ

DUA ISIYOKATALIWA

Mtunzi:

Sheikh Abdul Razzaaq Al-Badr

(Allaah amhifadhi)

Tarjama:

Abu Halima Arafat

(Allaah amsamehe yeye na wazazi wake)

بسم الله الرحمن الرحيم

Kila sifa njema anastahiki Alaah Mola Mlezi wa viumbe wote, -swala na salamu zimshukie- Mtume wetu Muhammad mbora wa Manabii na mwisho wa Mitume, na (ziwashukie) Jamaa zake na Maswahaba wote.

Baada ya hayo:

Hakika Allaah katika aya nyingi ndani ya kitabu chake amewaamrisha waja wake kuomba dua na akawaahidi kuwaitikia (kuwajibu).

Allaah amesema:

﴿وَقَالَ رَبُّكُمُ ٱدۡعُونِيٓ أَسۡتَجِبۡ لَكُمۡۚ إِنَّ ٱلَّذِينَ يَسۡتَكۡبِرُونَ عَنۡ عِبَادَتِي سَيَدۡخُلُونَ جَهَنَّمَ دَاخِرِينَ﴾

“Na Mola wenu Mlezi amesema: Niombeni nitakuitikieni. Hakika wale ambao wanafanya kibri kuacha kuniomba mimi wataingia Jahannamu hali ya kuwa madhalili[1]”.

Na amesema tena:

﴿إِنَّ رَبِّي لَسَمِيعُ ٱلدُّعَآءِ﴾

“Hakika Mola wangu Mlezi ni mwenye kuitikia dua[2]”.

[1]- Surat Ghafir/60.
[2]- Surat Ibrahim/39.

Na pia amesema:

﴿وَإِذَا سَأَلَكَ عِبَادِي عَنِّي فَإِنِّي قَرِيبٌ أُجِيبُ دَعْوَةَ الدَّاعِ إِذَا دَعَانِ فَلْيَسْتَجِيبُوا لِي وَلْيُؤْمِنُوا بِي لَعَلَّهُمْ يَرْشُدُونَ﴾

“Na watakapokuuliza waja wangu kuhusu mimi (waambie) mimi nipo karibu. Ninaitikia maombi ya mwombaji pindi akiniomba. Basi na waniitikie mimi na waniamini, ili wapate kuongoka[3]”.

Na amesema:

﴿ادْعُوا رَبَّكُمْ تَضَرُّعًا وَخُفْيَةً إِنَّهُ لَا يُحِبُّ الْمُعْتَدِينَ ** وَلَا تُفْسِدُوا فِي الْأَرْضِ بَعْدَ إِصْلَاحِهَا وَادْعُوهُ خَوْفًا وَطَمَعًا إِنَّ رَحْمَتَ اللَّهِ قَرِيبٌ مِنَ الْمُحْسِنِينَ﴾

“Muombeni Mola wenu Mlezi hali ya unyenyekevu na kwa siri. Kwa sababu yeye (Allaah) hawapendi wenye kuvuka mipaka** Wala msifanye uharibifu katika nchi baada ya kuwa imekwisha tengenezwa na muombeni yeye (Allaah) hali ya kumuogopa na kutumai. Hakika rehma za Allaah zipo karibu na wenye kutenda wema[4]”.

[3]- Surat Al-Baqara/186.
[4]- Surat Al-A’raaf/55-56.

Na hakika Allaah ‘Azza Wajalla amewahimiza waja wake kuomba dua pamoja na kujitosheleza kwake na kutowahitajia wao wala dua zao, kama alivyosema ‘Azza Wajalla kwenye hadithi Al-Qudsi:

«يَا عِبَادِيْ إِنَّكُمْ لَنْ تَبْلُغُوا ضَرِّي فَتَضُرُّونِي وَلَنْ تَبْلُغُوا نَفْعِيْ، فَتَنْفَعُونِيْ، يَا عِبَادِيْ لَوْ أَنَّ أَوَّلَكُمْ وَآخِرَكُمْ وَإِنْسَكُمْ وَجِنَّكُمْ كَانُوا عَلَى أَتْقَى قَلْبِ رَجُلٍ وَاحِدٍ مِنْكُمْ، مَا زَادَ ذَلِكَ فِيْ مُلْكِيْ شَيْئًا، يَا عِبَادِيْ لَوْ أَنَّ أَوَّلَكُمْ وَآخِرَكُمْ وَإِنْسَكُمْ وَجِنَّكُمْ كَانُوا عَلَى أَفْجَرِ قَلْبِ رَجُلٍ وَاحِدٍ، مَا نَقَصَ ذَلِكَ مِنْ مُلْكِيْ شَيْئًا، يَا عِبَادِيْ لَوْ أَنَّ أَوَّلَكُمْ وَآخِرَكُمْ وَإِنْسَكُمْ وَجِنَّكُمْ قَامُواْ فِيْ صَعِيدٍ وَاحِدٍ فَسَأَلُوْنِيْ فَأَعْطَيْتُ كُلَّ إِنْسَانٍ مَسْأَلَتَهُ، مَا نَقَصَ ذَلِكَ مِمَّا عِنْدِيْ إِلَّا كَمَا يَنْقُصُ الْمِخْيَطُ إِذَا أُدْخِلَ الْبَحْرَ .....»

“Enyi waja wangu, hamtanifika mimi na madhara mkanidhuru, wala hamtanifika mimi na manufaa mkaninufaisha.

Enyi waja wangu, lau wa mwanzo wenu na wa mwisho wenu, na watu wenu na majini, wangelikuwa juu ya uchaji wa moyo wa mtu mmoja miongoni mwenu, lisingezidisha hilo katika ufalme wangu chochote.

Enyi waja wangu, lau wa mwanzo wenu na wa mwisho wenu, na watu wenu na majini wenu wangelikuwa juu ya uovu wa moyo wa mtu mmoja, lisingepunguza hilo katika Ufalme wangu kitu chochote.

Enyi waja wangu, lau wa mwanzo wenu na wa mwisho wenu, na watu wenu na majini wenu, wangesimama katika uwanja mmoja wakaniomba mimi, kisha nikampatia kila mtu alichokiomba, lisingepunguza hilo kile kilicho kwangu isipokuwa kama (kiasi) inachopunguza sindano inapotoswa katika bahari.[5]”.

[5]- Sahihi Muslim (2577).

Naye yeye Allaah ‘Azza Wajalla pamoja na kutohitajia (kwao chochote) anapenda waja wake wamuombe, na kila mja anapopatiliza kuuomba dua ndipo kinapozidi cheo na daraja yake katika kupendwa na Allaah, mpaka Mtume -swala na salamu zimshukie- amesema:

"لَيْسَ شَيْءٌ أَكْرَمَ عَلَى اللهِ تَعَالَى مِنَ الدُّعَاءِ"

“Hakuna ibada iliyo bora zaidi mbele za Allaah Ta’alaa kuliko dua[6]”.

Na amesema:

"إِنَّهُ مَنْ لَمْ يَسْأَلِ اللَّهَ يَغْضَبْ عَلَيْهِ"

“Hakika asiyemuomba Allaah (chochote), (Allaah) anamchukia[7]”.

(Na Mshairi mmoja amesema:)

اللهُ يَغْضَبُ إِنْ تَرَكْتَ سُؤَالَهُ *** وَبُنَيَّ آدَمَ حِيْنَ يُسْأَلُ يَغْضَبُ

“Allaah anachukia ukiacha kumuomba * na mwanadamu akiombwa huchukia”

[6]- Sunan Tirmidh (3370). Amesema Sheikh Albani -Allaah amrehemu- kuwa hadithi hii ni Hasan.
[7]- Sunan Tirmidh (3373). Ameisahihisha Sheikh Albani -Allaah amrehemu-.

Kwa hiyo (Allaah) Mola wa viumbe wote anawapenda wenye kumuomba, na amewapa ahadi ya kujibu dua zao, kutimiza matarajio yao, na kuwapa wao matakwa yao; endapo yakitimia katika dua yao masharti ya kisheria, na kukosekana vizuizi.

(Kwa sababu) dalili nyingi za kisheria ndani ya Qur'an na Hadithi za Mtume -swala na salamu zimshukie- zimefahamisha kwamba dua yenye kujibiwa ina kanuni ambazo inampasa mwenye kuomba azizingatie wakati wa kuomba kwake, kadhalika kuna mikingamo (vizuizi) ambavyo ni wajibu wake kuviepuka, ili isije dua yake kukataliwa.

Na imam Ibnul Qayyim -Allaah amrehemu- amekusanya ufupisho mzuri uliokusanya kheri nyingi, amebainisha ndani yake yaliyo muhimu katika yale ambayo inapasa wenye kuomba kuyazingatia katika kumuomba kwao Allaah, kisha baada ya kutaja masharti hayo alihitimisha maneno yake kwa kusema:

"فَإِنَّ هَذَا الدُّعَاءَ لَا يَكَادُ يُرَدُّ أَبَدًا"

"Kwa hakika dua hii haikurubii kabisa kukataliwa[8]".

Ikawa miongoni mwa nasaha na kheri ni kueneza maneno yake na kuyafafanua kwa kile ambacho kitabainisha makusudio yake na

[8]- Kitabu: [Al-jawaabul Kaafi], (Uk: 9).

kukuza faida yake, na hapa nitayataja maneno yake yote. Amesema Ibnul Qayyim -Allaah amrehemu-:

وَإِذَا جَمَعَ مَعَ الدُّعَاءِ حُضُورَ الْقَلْبِ وَجَمْعِيَّتَهُ بِكُلِّيَّتِهِ عَلَى الْمَطْلُوبِ، وَصَادَفَ وَقْتًا مِنْ أَوْقَاتِ الْإِجَابَةِ السِّتَّةِ، وَهِيَ: الثُّلُثُ الْأَخِيرُ مِنَ اللَّيْلِ، وَعِنْدَ الْأَذَانِ، وَبَيْنَ الْأَذَانِ وَالْإِقَامَةِ، وَأَدْبَارُ الصَّلَوَاتِ الْمَكْتُوبَاتِ، وَعِنْدَ صُعُودِ الْإِمَامِ يَوْمَ الْجُمُعَةِ عَلَى الْمِنْبَرِ حَتَّى تُقْضَى الصَّلَاةُ مِنْ ذَلِكَ الْيَوْمِ، وَآخِرُ سَاعَةٍ بَعْدَ الْعَصْرِ. وَصَادَفَ خُشُوعًا فِي الْقَلْبِ، وَانْكِسَارًا بَيْنَ يَدَيِ الرَّبِّ، وَذُلًّا لَهُ، وَتَضَرُّعًا، وَرِقَّةً. وَاسْتَقْبَلَ الدَّاعِي الْقِبْلَةَ. وَكَانَ عَلَى طَهَارَةٍ. وَرَفَعَ يَدَيْهِ إِلَى اللَّهِ. وَبَدَأَ بِحَمْدِ اللَّهِ وَالثَّنَاءِ عَلَيْهِ. ثُمَّ ثَنَّى بِالصَّلَاةِ عَلَى مُحَمَّدٍ عَبْدِهِ وَرَسُولِهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ. ثُمَّ قَدَّمَ بَيْنَ يَدَيْ حَاجَتِهِ التَّوْبَةَ وَالِاسْتِغْفَارَ. ثُمَّ دَخَلَ عَلَى اللَّهِ، وَأَلَحَّ عَلَيْهِ فِي الْمَسْأَلَةِ، وَتَمَلَّقَهُ وَدَعَاهُ رَغْبَةً وَرَهْبَةً. وَتَوَسَّلَ إِلَيْهِ بِأَسْمَائِهِ وَصِفَاتِهِ وَتَوْحِيدِهِ. وَقَدَّمَ بَيْنَ يَدَيْ دُعَائِهِ صَدَقَةً، فَإِنَّ هَذَا الدُّعَاءَ لَا يَكَادُ يُرَدُّ. أَبَدًا وَلَا سِيَّمَا إِنْ صَادَفَ الْأَدْعِيَةَ الَّتِي أَخْبَرَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ أَنَّهَا مَظِنَّةُ الْإِجَابَةِ، أَوْ أَنَّهَا مُتَضَمِّنَةٌ لِلِاسْمِ الْأَعْظَمِ.

“Akikusanya pamoja na dua yake, kuhudhuria kwa moyo na kukusanyika kwake wote juu ya kile anachoomba, na ikasadifu wakati miongoni mwa nyakati sita za kujibiwa dua, ambazo ni:

1. Thuluthu ya mwisho ya usiku.
2. Wakati wa Adhana.
3. Baina ya Adhana na Iqama.
4. Mwishoni mwa swala za faradhi (kabla ya kutoa salamu) .
5. Wakati imamu akipanda juu ya mimbari siku ya Ijumaa mpaka kuswaliwa swala ya Ijumaa.

6. Na wakati wa mwisho baada ya swala ya Alasiri[9].
    1. Na ikasadifu unyenyekevu wa moyo, kujipendekeza mbele ya Allaah na kudhalilika pamoja na kuwa laini.
    2. Akaelekea mwombaji upande wa kibla.
    3. Akawa yuko twahara.
    4. Akanyanyua mikono kuelekea kwa Allaah.
    5. Akaanza kwa kumhimidi Allaah na kumsifu-.
    6. Kisha akamswalia Mtume Muhammad.
    7. Kisha akatanguliza katika haja yake hiyo toba na msamaha.
    8. Kisha akaingia kwa Allaah, akabembeleza katika maombi yake na akajipendekeza.
    9. Na akaomba hali ya kuwa na matumaini na khofu.
    10. Na akatawasali kwake kwa majina, sifa, na tauhid yake.
    11. Na akatanguliza katika dua yake hiyo sadaka. Hakika dua (ya namna) hii haikurubii kabisa kukataliwa.
    12. Hasahasa ikisadifu dua ambazo Mtume -swala na salamu zimshukie- ameelezea kuwa dua hizo ni mahala pa kudhaniwa kujibiwa au (dua ambazo) zimekusanya jina la Allaah tukufu[10].

[9]- Baina ya Alasiri na Maghrib hapo katikati yake kuna kitambo kidogo ambacho Dua inajibiwa.
[10]- Kitabu: Al-Jawaabul Kaafi] (Uk. 16-18).

Jambo la kwanza

"حُضُورُ الْقَلْبِ وَاجْتِمَاعُهُ عَلَى الْمَطْلُوبِ"

“Kuhudhuria kwa moyo na kukusanyika kwake (wote) juu ya anachokiomba”.

Jambo la kwanza ni: Kuomba muislamu kwa moyo wenye kuhudhuria, na kuhudhuria kwa moyo ni: ni kuelekea kwake kwa Allaah, isiwe dua yake ni kwa kutikisa ulimi tu hali ya kuwa moyo wake (uko mbali) umeghafilika, lakini atikise ulimi akiomba dua pamoja na kuhudhurisha moyo, kwa ajili hii amesema Mtume -swala na salamu zimshukie-:

"ادْعُوا اللَّهَ وَأَنْتُمْ مُوقِنُونَ بِالإِجَابَةِ، وَاعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ لاَ يَسْتَجِيبُ دُعَاءً مِنْ قَلْبٍ غَافِلٍ لاَهٍ"

“Muombeni Allaah na hali ya kuwa nyinyi mna yakini kuwa mtajibiwa, na tambueni kwamba Allaah hajibu dua yoyote kutoka kwenye moyo wenye kughafilika wenye pumbao[11]”.

Na miongoni mwa alama za kutohudhuria moyo wakati wa dua ni kushughulika na kuwa harakati nyingi wakati wa kuomba dua, utapata (mtu) ulimi wake unatikisika kwa kuomba dua lakini mikono yake inachezea mchanga au udongo n.k, au utampata anageuza macho yake kulia na kushoto wakati wa kuomba dua, hayo yote ni kwa sababu moyo haukukusanyika kwa Allaah wakati wa dua. Kwa ajili hiyo wakati Omar Bin Abdil Aziz -Allaah

[11]- Sunan Tirmidh (3479). Amesema Sheikh Albani -Allaah amrehemu- kuwa hadithi hii ni Hasan.

amrehemu-alipomuona mtu mmoja anamuomba Allaah hali ya kuwa mkononi mwake kuna changarawe anazichezea alimwambia:

"أَلَا أَلْقَيْتَ الْحَصَاةَ، وَأَخْلَصْتَ إِلَى اللهِ الدُّعَاءَ"

"Kwanini usitupe (hizo) changarawe ukamtakasia Allaah dua?!"[12][13].

Na imepatikana katika zama hizi aina mpya ya changarawe wakati mwingi ziko mikononi mwa watu, zimeishughulisha zaidi mioyo kuliko mikono kwa kukusanya rundo kubwa la mchezo na pumbao, basi (haikuweza) tena mioyo kurudi kufanya vizuri katika maombi, wala kunyenyekea na kuomba dua, na watu hao ni haki yake kuambiwa: **"Kwanini usizime simu na ukamtakasia Allaah maombi?!".**

Kwa hiyo jambo la kwanza kwa anayetaka kujibiwa dua yake na Allaah ni amuelekee Allaah kwa moyo wake wote wakati wa kuomba, na apambane na nafsi yake katika kuukusanya moyo na fikra zake juu ya anachokiomba na kukihitaji, wala asiushughulishe (moyo) tafauti na anachomuomba Mola wake, kwa sababu moyo ukiachwa unatawanyika, ni lazima kupambana katika kuukusanya na kuuhudhurisha wakati wa kuomba.

[12]- Kitabu: [Hilyatul Auliyaa] cha Abu Nu'aim -Allaah amrehemu-.
[13]- Kwanini usiache kuchezea hizo changarawe na badala yake ukamuelekea Allaah tu pakee?.

Jambo la pili:

"تَحَرِّيْ أَوْقَاتِ الْإِجَابَةِ"

“Kufanya pupa (kupatiliza) nyakati zenye kujibiwa”.

Na imam Ibnul Qayyim -Allaah amrehemu- amezitaja sehemu sita, miongoni wa hizo:

1. **Thuluthi ya mwisho katika usiku:** na unazingatiwa kuwa ni miongoni mwa nyakati zenye kutarajiwa zaidi kujibiwa dua, na ndio wenye utukufu zaidi, kwa hadithi iliyotajwa katika sahihi mbili, Mtume -swala salamu zimshukie- amesema:

"يَنْزِلُ رَبُّنَا تَبَارَكَ وَتَعَالَى كُلَّ لَيْلَةٍ إِلَى السَّمَاءِ الدُّنْيَا حِينَ يَبْقَى ثُلُثُ اللَّيْلِ الآخِرُيَقُولُ: مَنْ يَدْعُونِيْ، فَأَسْتَجِيبَ لَهُ مَنْ يَسْأَلُنِيْ فَأُعْطِيَهُ، مَنْ يَسْتَغْفِرُنِيْ فَأَغْفِرَلَهُ"

“Mola wetu aliyetukuka anateremka kila usiku mpaka kwenye mbingu ya dunia wakati inapobaki thuluthi ya mwisho ya usiku anasema: Nani anaeniomba (dua) ili nimjibu?, Nani anaeniomba kitu ili nimpatie?, Nani anaeniomba msamaha ili nimsamehe?[14]”.

Hadithi hii imefahamisha kwamba wakati huu mtukufu uliobarikiwa ndio wakati wenye kutarajiwa zaidi kukubaliwa dua, (kwa hiyo) inapasa kwa muislamu ajitahidi kuipata kheri hii, na afanye pupa (juu ya) kwamba usimpite usiku wowote isipokuwa amuomba Allaah Ta’alaa katika wakati huo.

[14]- Bukhari (1145) na Muslim (758).

2. Baada ya Adhana:

Baada tu ya kumalizika adhana, huu ni wakati bora sana wa kujitahidi kuomba, kwa sababu hadithi zimefahamisha juu ya kwamba mwenye kusikiliza adhana, akaitikia (kwa kumfuatisha) muadhini[15] kisha baada ya hapo akaomba, basi dua yake ni yenye kukubaliwa.

Imepokewa na Ibn Umar -Allaah amridhie- kwamba mtu mmoja alimwambia Mtume -swala na salamu zimshukie-: **Ewe Mtume wa Allaah, Waadhini wametutangulia katika fadhila.** Akasema:

«قُلْ كَمَا يَقُولُونَ فَإِذَا انْتَهَيْتَ فَسَلْ تُعْطَهْ»

"Sema kama wanavyosema (wao) na utakapomaliza omba utapewa[16]".

Hadithi hii imefahamisha juu ya mafungamano ya fadhila za dua hii kwa kusikiliza adhana na (kuitikia kwa) kumfuatisha muadhini, kwa hiyo inapasa kwa muislamu pindi anaposikia adhana na kuitikia matamko yake kwa kumuiga mudhini, na akafuatishia kile kilichothibiti katika sunna, ambacho ni kumswalia Mtume -swala na salamu zimshukie- na kumuombea yeye kwa Allaah wasila na fadhila, basi afuatishie kwa kuomba kile

---

[15]- Isipokuwa katika neno : **(Hayya alas swalaaat, Hayya alal falaah:** (حَيَّ عَلَى الصَّلَاةِ حَيَّ عَلَى الْفَلَاحِ), atasema: **(Laa Haula wala Quwwata illaa Billaah:** لَا حَولَ وَلَا قُوَّةَ إِلَّا بِالله **)**

[16]- Sunan Abi Daud (524). Na Sheikh Albani ameihukumu kuwa ni Hasan.

anachotaka kwa sababu huo ni wakati bora wenye kutarajiwa kujibiwa.

3. Baina ya Adhana na Iqama:

Kuna matamko mengi ya kisheria yameelezea fadhila ya kuomba dua katika wakati wa baina ya Adhana na Iqama, miongoni mwake ni kauli ya Mtume -swala na salamu zimshukie-:

«الدُّعَاءُ لَا يُرَدُّ بَيْنَ الْأَذَانِ وَالْإِقَامَةِ»

"Dua baina ya Adhana na Iqama hairudishwi[17]".

Na amesema Mtume -swala na salamu zimshukie-:

«إِذَا نُودِيَ بِالصَّلَاةِ، فُتِحَتْ أَبْوَابُ السَّمَاءِ، وَاسْتُجِيبَ الدُّعَاءُ»

"Inapoadhiniwa kwa ajili ya swala milango ya mbingu inafunguliwa, na dua zinajibiwa[18]".

Kwa hiyo inapasa kwa muislamu katika wakati huo akithirishe kujiombea dua na kumuomba Allaah kheri.

4. Mwishoni mwa swala ya faradhi (kabla ya kutoa salamu) :

Kwa hakika wakati huo ni bora na unatarajiwa zaidi kujibiwa mwombaji dua, kwa sababu zimekusanyika ndani yake sababu nyingi za kujibiwa dua, kwa sababu muislam anakuwa amejitwaharisha, mwenye kuelekea kibla, anapiga Takbira

[17]-Sunan Abi Daud (4913). Ameisahihisha Sheikh Albani katika kitabu: [Ir'waaul Ghalili] (224).
[18]- Kitabu: [Musnad Twayaalisiy] (524), na ameisahihisha Sheikh Albani katika: [As-Sahiiha] (1413).

(akamtukuza Allaah) , anasoma sehemu katika Qur'an, kisha anarukuu na kusujudu kwa ajili ya kumnyenyekea Allaah, kisha baada ya hapo anakaa kikao cha tashah'ud, na kuanza kwa kusoma (At-Tahiyyaat) na kumswalia Mtume -swala na salamu zimshukie- kwa ukamilifu, (As-swalaatul Ibraahimiyyah) .

Mambo hayo yote ni miongoni mwa ibada ambazo zinaifanya sehemu (ya tashah'ud) kuwa ni sehemu yenye kutarajiwa zaidi kujibiwa dua za wenye kuswali, kwa sababu hii imekuja mwishoni mwa hadithi ya Ibn Masoud -Allaah amridhie- wakati Mtume -swala na salamu zimshukie- alipofundisha tashah'hud (akasema) :

«ثُمَّ يَتَخَيَّرُ مِنَ الدُّعَاءِ أَعْجَبَهُ إِلَيْهِ، فَيَدْعُو»

"Kisha achague katika dua ile inayompendeza zaidi aombe[19]".

5. Wakati wa kupanda imamu juu ya mimbari siku ya ijumaa:

Hili ni kwa hadithi inayosema:

«إِنَّ فِي الْجُمُعَةِ لَسَاعَةً، لَا يُوَافِقُهَا مُسْلِمٌ، قَائِمٌ يُصَلِّي، يَسْأَلُ اللهَ خَيْرًا، إِلَّا أَعْطَاهُ إِيَّاهُ»

"Hakika kuna katika siku ya Ijumaa muda (mdogo) ambao haudiriki (muda huo) muislamu yeyote hali ya kuwa ni mwenye kulazimiana na kuomba (dua), anamuomba Allaah kheri isipokuwa Allaah atampatia[20]".

[19]- Bukhari (835) na Muslim (402). Na tamko hili ni la imam Bukhari.
[20]- Bukhari (6400) na Muslim (852). Na tamko hili ni la imam Muslim.

Baadhi ya maulamaa wanaona kuwa muda huo ni baada ya imamu kupanda juu ya mimbari mpaka kukamilika swala ya ijumaa, kwa hadithi ya Abu Musa Al-ash'ariy -Allaah amridhie:-

«هِيَ مَا بَيْنَ أَنْ يَجْلِسَ الْإِمَامُ إِلَى أَنْ تُقْضَى الصَّلَاةُ»

"(Muda) huo ni baina ya anapokaa imamu juu ya mimbari mpaka kumalizika swala[21]".

Hadithi hii imepokewa na Abu Musa hali ya kuwa ni marfuu' (kuwa amesema Mtume) na vilevile imepokewa hali ya kuwa ni mauquuf (kuwa Abu Musa) ndiye aliesema, ndio maana kuna kundi la maulamaa wameipa nguvu kuwa muda wa kujibiwa dua upo katika wakati huo. Basi muislamu ajitahidi kuitikia dua ya khatibu (pindi anapoomba), na pia akithirishe siku ya ijumaa kuomba dua kwa wingi, kwa sababu muda huo wa kujibiwa unaendelea mpaka kumalizika swala, hasa wakati (anapokuwa) amesujudu:

«أَقْرَبُ مَا يَكُونُ الْعَبْدُ مِنْ رَبِّهِ، وَهُوَ سَاجِدٌ، فَأَكْثِرُوا الدُّعَاءَ»

"Wakati anapokuwa mja yu karibu zaidi na Mola wake hali anapokuwa amesujudu, basi kithirisheni (kuomba) dua[22]".

Kadhalika ajitahidi kuomba dua baada ya kumaliza tashah'ud (At-tahiyaat) na kabla imamu hajatoa salamu, kwa sababu hapo ni miongoni mwa sehemu za kujibiwa dua.

[21]- Muslim (853).
[22]- Muslim (482).

6. Wakati wa mwisho baada ya swala ya alasiri:

Wakati wa mwisho baada ya swala ya alasiri siku ya ijumaa mpaka kuzama kwa jua, Mtume -swala na salamu zimshukie- amesema:

«يَوْمُ الْجُمُعَةِ ثِنْتَا عَشْرَةَ، يُرِيدُسَاعَةً، لاَ يُوجَدُ مُسْلِمٌ يَسْأَلُ اللَّهَ عَزَّوَجَلَّ شَيْئًا، إِلاَّ أَتَاهُ اللَّهُ عَزَّوَجَلَّ، فَالْتَمِسُوْهَا آخِرَسَاعَةٍ بَعْدَ الْعَصْرِ».

"Siku ya ijumaa ni masaa kumi na mbili, anaukusudia muda ambao hapatikani muislamu yeyote anaemuomba Allaah 'Azza Wajalla kitu chochote (katika kheri za dunia na akhera), isipokuwa Allaah atampa, basi utafuteni (muda) huo wakati wa mwisho baada ya alasiri[23]".

Kwa ajili hiyo ametaja mwanachuoni mkubwa Ibnul Qayyim -Allaah amrehemu- kwamba kauli yenye nguvu na yenye kutarajiwa zaidi katika kuweka ukomo wa muda wenye fadhila siku ya ijumaa, ambao dua hujibiwa, ni kauli hizo mbili zilizotangulia: (1) Imamu anapopanda juu ya mimbari mpaka kumalizika swala. (2) Muda wa mwisho siku ya ijumaa, alasiri mpaka kuzama kwa jua[24].

Kwa hiyo inapasa kwa muislamu mwenye kuinasihi nafsi yake ajitahidi zisimpite nyakati hizi mbili zenye fadhila, na kuzihusisha kwa kumuomba Allaah ziada ya fadhila ili aipate kheri ambayo anaitaka na kuitarajia kwa Allaah Mola wa viumbe.

[23]- Sunan Abi Daud (1048). Na ameisahihisha Sheikh Albani katika Sahihi Sunan Abi Daud (966).
[24]- Zaadul Maad (Jz. 1, Uk. 377)

Jambo la Tatu

<<خُشُوعُ الْقَلْبِ، وَانْكِسَارُهُ بَيْنَ يَدَيِ رَبِّهِ، ذُلًّا وَتَضَرُّعًا>>

“Unyenyekevu wa moyo na kudhalilika kwake mbele ya Allaah”.

Jambo (hili) alilotaja Ibnul Qayyim -Allaah amrehemu- lina umuhimu mkubwa wakati wa kuomba dua na pia kwenye ibada nyingine, kwa sababu miongoni mwa kutimiza utumwa kwa Allaah ni mja kuwa dhalili na kunyenyekea kwa muumba wake, hasa hasa wakati wa dua na kuomba, kama alivyosema Allaah:

﴿ٱدۡعُواْ رَبَّكُمۡ تَضَرُّعٗا وَخُفۡيَةًۚ إِنَّهُۥ لَا يُحِبُّ ٱلۡمُعۡتَدِينَ﴾

“Muombeni Mola wenu Mlezi kwa unyenyekevu na kwa siri. Hakika yeye hawapendi wenye kuvuka mipaka”.

Amesema imam At-Twabari -Allaah amrehemu-: **“(تَضَرُّعًا) ni udhalili na kutii, na (خُفْيَةً): kwa unyenyekevu wa mioyo yenu[25]”.**

Kwa hiyo inapasa kwa mwombaji wakati wa kuomba kwake aonyeshe unyenyekevu na udhalili mbele ya Mola wake, na amuite kwa sauti ya chini kwa heshima na adabu, ndio pale Mtume alipowaona baadhi ya Maswahaba -Allaah awaridhie- wakinyanyua sauti zao kwa kusoma dhikri na dua akasema:

[25]- Kitabu: [Jaamiul bayaan fii tafsiiril Qur’an]. (Jz. 10, Uk. 247).

«أَيُّهَا النَّاسُ ارْبَعُوا عَلَى أَنْفُسِكُمْ، إِنَّكُمْ لَيْسَ تَدْعُونَ أَصَمَّ وَلاَ غَائِبًا، إِنَّكُمْ تَدْعُونَ سَمِيعًا قَرِيبًا، وَهُوَ مَعَكُمْ»

“Enyi watu, zihurumieni nafsi zenu, kwa sababu hamkuwa nyinyi mnamuomba kiziwi wala aliye mbali, hakika nyinyi mnamuomba Mwenye kusikia Aliye karibu, naye yuko pamoja na nyinyi[26]”.

Amesema Ibn Hajar -Allaah amrehemu-, amesema At-Twabari:

«فِيهِ كَرَاهِيَةُ رَفْعِ الصَّوْتِ بِالدُّعَاءِ وَالذِّكْرِ وَبِهِ قَالَ عَامَّةُ السَّلَفِ مِنَ الصَّحَابَةِ وَالتَّابِعِينَ»

“Kuna katika hadithi hii karaha ya kunyanyua sauti kwa kuleta dua na dhikri, na kwa (kauli) hiyo wamesema (maulamaa) wote wa Salaf katika Maswahaba na Taabi’na[27]”.

Na imamu Nnawawi -Allaah amrehemu- ameiwekea hadithi hii mlango unaosema:

«بَابُ اسْتِحْبَابِ خَفْضِ الصَّوْتِ بِالذِّكْرِ إِلَّا فِي الْمَوَاضِعِ الَّتِيْ وَرَدَ الشَّرْعُ بِرَفْعِهِ فِيْهَا»

“Huu ni mlango wa kupendekezwa kuteremsha sauti kwa ajili ya (kusoma) dhikri isipokuwa katika sehemu ambazo sheria imeidhinisha kunyanyua sauti katika sehemu hizo[28]”.

[26]- Bukhari (2992) na Muslim (2704) na hili ni tamko la Muslim.
[27]- Kitabu: [Fat’hul Baari] (Jz. 6, Uk. 135). Ibn Hajar.
[28]- Kitabu: [Sharhu sahihi Muslim] (Jz. 17, Uk. 25).

Jambo la Nne:

<<اسْتَقْبَالُ الْقِبْلَةِ وَقْتَ الدُّعَاءِ>>

“Kuelekea upande wa kibla wakati wa kuomba dua”

Kuelekea kibla wakati wa kuomba dua ni miongoni mwa mambo yenye kuzingatiwa kuwa ni adabu kubwa wakati wa kuomba (dua) , ambayo inafahamisha juu ya kuiadhimisha kwake mwombaji (dua) na kuipa umuhimu wake.

Ndiyo maana imethibiti kutoka kwa Mtume -swala na salamu zimshukie- alikuwa anaelekea kibla kisha anaomba dua, kama ilivyotokea katika vita vya Badri wakati alipoona idadi kubwa ya (jeshi la) washirikina dhidi ya (jeshi la) waislamu:

«فَاسْتَقْبَلَ نَبِيُّ اللهِ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ الْقِبْلَةَ، ثُمَّ مَدَّ يَدَيْهِ»

“Mtume -swala na salamu zimshukie- akaelekea kibla kisha akanyanyua mikono yake[29] (akaomba).

Hilo ni kwa sababu kuelekea mwombaji upande wa kibla ni miongoni mwa sababu ambazo hutarajiwa pamoja nayo kujibiwa dua yake, jambo hilo si katika masharti ya dua lakini ni miongoni mwa adabu zake zilizo nzuri.

[29]- Muslim (1763).

Jambo la Tano

<<الطَّهَارَةُ عِنْدَ الدُّعَاءِ>>

“Kuwa twahara wakati wa kuomba dua”.

Kuwa na twahara pia ni miongoni mwa adabu za dua, wala hapana shaka kwamba mwombaji anapokuwa twahara ni bora na ukamilifu zaidi kwa ajili ya maombi yake na kumnong’oneza kwake Allaah, kwa sababu kuwa katika udhu ni bora kuliko kuwa katika hadathi.

Imepokewa kutoka kwa Muhajir Ibn Qunfudh -Allaah amridhie-, kwamba yeye alimsalimia Mtume -swala na salamu zimshukie- hali ya kuwa anatawadha, hamuitikia, mpaka alipomaliza kutawadha alimwambia:

«إِنَّهُ لَمْ يَمْنَعْنِيْ أَنْ أَرُدَّ عَلَيْكَ إِلَّا أَنِّي كَرِهْتُ أَنْ أَذْكُرَ اللهَ إِلَّا عَلَى طَهَارَةٍ»

“Hakika hakuna kilichonizuia mimi kukuitikia wewe isipokuwa mimi nimechukia kumtaja Allaah isipokuwa nikiwa katika twahara[30]”.

[30]- Abu Daud (18), na Ahmad (19034), na tamko hili ni lake. Tazama [As sahiha] (834). Sheikh Albani.

Jambo la Sita:

<<رَفْعُ اليَدَيْنِ عِنْدَ الدُّعَاءِ>>

“Kunyanyua mikono wakati wa kuomba dua”

Imepokewa kutoka kwa Salman Al-Farisiy -Allaah amridhie-, kwamba Mtume -swala na salamu zimshukie- amesema:

«إِنَّ رَبَّكُمْ تَبَارَكَ وَتَعَالَى حَيِيٌّ كَرِيمٌ، يَسْتَحْيِي مِنْ عَبْدِهِ إِذَا رَفَعَ يَدَيْهِ إِلَيْهِ، أَنْ يَرُدَّهُمَا صِفْرًا»

“Hakika Mola wenu Mlezi ni Mwenye haya (na) Mkarimu, anamuonea haya mja wake pindi anaponyanyua mikono yake kuilekeza kwake kuirudisha sifuri (haina kitu/mitupu)[31]”

Allaah ni mkwasi, anamuonea haya mja wake pindi akinyanyua mikono yake kuirudisha patupu, hilo ni kwa sababu kunyanyua mikono kwa kuelekeza matumbo ya viganja vyake mbinguni au mkabala na uso wake (mwombaji), namna hii huzingatiwa ni sura ya uhitaji, udhalili na kukatikiwa, na kuonyesha ufakiri na kuhitajia, ikawa hilo ni miongoni mwa sababu za kujibiwa dua na Allaah.

Na hadithi ambazo zinaonyesha kwamba Mtume -swala na salamu zimshukie- akinyanyua mikono wakati wa kuomba dua ni nyingi, na wakati wa shida na majanga alikuwa ananyua mikono yake zaidi,

[31]- Abu Daud (1488) na ameisahihisha Sheikh Albani.

kama ilivyotangulia (kutajwa) katika vita vya Badri wakati alipoona idadi kubwa ya (jeshi la) makafiri dhidi waislamu, alielekea kibla, kisha akanyanyua mikono yake na akamuomba Mola wake.

Amesema Omar Ibnul Khatwaab -Allaah amridhie-:

«فَمَا زَالَ يَهْتِفُ بِرَبِّهِ، مَادًّا يَدَيْهِ مُسْتَقْبِلَ الْقِبْلَةِ، حَتَّى سَقَطَ رِدَاؤُهُ عَنْ مَنْكِبَيْهِ»

“Hajaacha kuwa anamuomba Mola wake (kuokolewa), hali ya kuwa ni Mwenye kunyanyua mikono yake, Mwenye kuelekea (upande wa) kibla, mpaka kikadondoka kishali chake kutoka mabegani mwake[32]”.

Na vilevile wakati wa ukame pindi Mtume -swala na salamu zimshukie- alipoomba dua ya kutaka kunyeshelezwa mvua akiwa juu ya mimbari. Amesema Anas Bin Malik -Allaah amridhie-:

«رَأَيْتُ رَسُولَ اللهِ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَرْفَعُ يَدَيْهِ فِي الدُّعَاءِ، حَتَّى يُرَى بَيَاضُ إِبْطَيْهِ»

“Nilimuona Mtume -swala na salamu zimshukie- ananyanyua mikono yake katika kuomba dua, mpaka unaonekana weupe wa kwapa zake[33]”.

[32]- Muslim (1763).
[33]- Bukhari (1030) na Muslim (895), na hili ni tamko la Muslim.

Jambo la Saba:

<<البَدَاءَةُ بِحَمْدِ اللهِ وَتَمْجِيْدِهِ ثُمَّ الصَّلَاةُ عَلَى نَبِيِّهِ مُحَمَّدٍ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَبْلَ الدُّعَاءِ>>

“Kuanza kwa kumhimidi Allaah na kumtukuza yeye kisha kumswalia Mtume Muhammad -swala na salamu zimshukie- kabla ya kuomba dua”.

Imepokewa kutoka kwa Fudhwala Bin Ubeid -Allaah amridhie- amesema: Mtume -swallaLlaahu alaihi wasallam- alimsikia mtu mmoja anaomba katika swala yake, hakumtukuza Allaah Ta’alaa wala hakumswalia Mtume -swallaLlaahu alaihi wasallam-, akasema Mtume -swallaLlaahu alaihi wasallam- akasema:

«عَجِلَ هَذَا»

“Amefanya haraka huyu”.

Kisha akamwita na akamwambia:

«إِذَا صَلَّى أَحَدُكُمْ، فَلْيَبْدَأْ بِتَمْجِيدِ رَبِّهِ جَلَّ وَعَزَّ، وَالثَّنَاءِ عَلَيْهِ، ثُمَّ يُصَلِّي عَلَى النَّبِيِّ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ، ثُمَّ يَدْعُو بَعْدُ بِمَا شَاءَ».

“Ataposwali mmoja wenu, aanze kumtukuza Mola wake ‘Azza Wajalla (hali ya kuwa ametukuka na mwenye kushinda), na amsifu, kisha amswalie Mtume -swala na salamu zimshukie-, kisha baada ya hapo aombe kile anachotaka[34]”.

Ukamilifu ni kuwa muislamu anapoingilia kuomba dua atangulize kumsifu Allaah, kumtukuza na kisha afuatishie kumswalia Mtume -swala na salamu zimshukie-, kisha baada ya hapo amuombe Mola wake kile anachokipenda.

Na kwa ajili hii tunapata kufahamu fadhila za kuomba dua baada ya kusikia adhana, na pia baada ya tashah’ud ya mwisho katika swala, kwa sababu katika sehemu zote hizi mbili kunatangulia kusifiwa Allaah na kutukuzwa, na kumswalia Mtume -swala na salamu zimshukie-, ikanasibiana kuwa dua baada ya sehemu hizo mbili ni mahala pa kujibiwa.

[34]- Abu Daud (1481) na Tirmidh (3477).

Jambo la Nane:

<<التَّوْبَةُ والاسْتِغْفَارُبَيْنَ يَدَيِ الدُّعَاءِ>>

“Toba na Istighfaar (kutaka msamaha) kabla ya dua”.

Hakika madhambi ni katika vizuizi vyenye kuathiri juu ya kujibiwa dua, kama ilivyothibiti kutoka kwa Mtume -swala na salamu zimshukie- wakati alipomtaja mtu ambaye:

«يُطِيلُ السَّفَرَ أَشْعَثَ أَغْبَرَ، يَمُدُّ يَدَيْهِ إِلَى السَّمَاءِ، يَا رَبِّ، يَا رَبِّ، وَمَطْعَمُهُ حَرَامٌ، وَمَشْرَبُهُ حَرَامٌ، وَمَلْبَسُهُ حَرَامٌ، وَغُذِيَ بِالْحَرَامِ، فَأَنَّى يُسْتَجَابُ لِذَلِكَ؟»

“Amesafiri safari ndefu[35], hali ya kuwa ametimka nywele, amejaa vumbi, hali ya kuwa ni mwenye kunyanyua mikono yake kuelekeza mbinguni, Yaa Rabbi, Yaa Rabbi (Ewe Mola wangu, Ewe Mola wangu), hali ya kuwa chakula chake ni haramu, kinywaji chake ni haramu, nguo zake ni haramu, na amekulia kwa haramu, basi kutokea wapi atajibiwa mtu huyo![36]”.

Zimekusanyika kwa mtu huyu sababu nyingi za kujibiwa dua yake, amemuomba Mola wake hali ya kuwa yumo safarini, amenyanyua mikono yake kuilekeza mbinguni, lakini hakujizuia na haramu,

[35]- Wanachuoni wanasema, safari ni sababu ya kujibiwa dua lakini isiwe safari ya kuiendea haramu
[36]- Muslim (1015).

nguo zake, chakula na kinywaji chake kimetokana na haramu, likawa hilo ni kizuizi cha kujibiwa dua yake.

Na amesema mmoja katika Salaf[37]:

«لَا تَسْتَبْطِئَنَّ الْإِجَابَةَ إِذَا دَعَوْتَ وَقَدْ سَدَدْتَ طُرُقَهَا بِالذُّنُوبِ»

“Usione kuchelewa kujibiwa pindi ukiomba na hali ya kuwa umeziba njia zake[38] kwa sababu ya madhambi[39]”.

Kwa ajili hiyo Mtume -swala na salamu zimshukie- alikuwa anamuomba Allaah msamaha na kutubia kwake kwa siku mara mia moja, na anawahimiza hilo umma wake, anasema:

«يَا أَيُّهَا النَّاسُ تُوبُوا إِلَى اللهِ، فَإِنِّي أَتُوبُ فِي الْيَوْمِ إِلَيْهِ مِائَةَ مَرَّةٍ»

“Enyi watu, tubieni kwa Allaah, kwa sababu mimi natubia kwake kwa siku mara mia moja[40]”.

Inapasa kwa muislamu mwenye kuinasihi nafsi yake akithirishe Istighfaar (kutaka msamaha) na toba, na kukiri madhambi, kujutia, na kuazimia kutorudia tena, hasa hasa wakati wa kumuomba Allaah, kwa hakika hilo ni sababu ya Allaah kumkubalia toba yake, na hupelekea zaidi kwenye kujibiwa dua na kupewa alichokiomba.

---

[37]- Maneno hayo ameyasema Abu Zakariyya Yahya Ibn Muadh Ar Raazi -Allaah amrehemu-.
[38]- Akikusudia kwamba madhambi ndio sababu na kizuizi kikubwa chenye kuzuia dua isijibiwe.
[39]- Kitabu: [Shu’abul Imaan] (1154).
[40]- Muslim (2702).

Jambo la Tisa:

<<الإِلْحَاحُ فِي الدُّعَاءِ وَعَدَمُ اسْتِعْجَالِ الإِجَابَةِ>>

”Kubembeleza[41] katika Dua na kutoharakisha kujibiwa”.

Imepokewa kutoka kwa Abu Huraira -Allaah amridhie- amesema:

«يُسْتَجَابُ لِأَحَدِكُمْ مَا لَمْ يَعْجَلْ، فَيَقُولُ: قَدْ دَعَوْتُ رَبِّيْ فَلَمْ يَسْتَجِبْ لِيْ»

“Hujibiwa mmoja wenu muda wa kuwa hajakata tamaa (akaacha kuomba), anasema: Nimemuomba Mola wangu wala hajanijibu[42]”.

Miongoni mwa adabu kubwa za dua ni kubembeleza (wakati) wa maombi, kuirejearejea dua na kudumu katika maombi, pamoja na kuvizia nyakati zenye fadhila, **kwa sababu mwenye kudumu kugonga mlango anakaribia kufunguliwa.**

Na yeyote mwenye kuzingatia dua za watu wema mwishoni mwa surat Aal-‘Imraan namna gani wao walivyokariri neno (Rabbanaa - رَبَّنَا) mara tano, ikaja mwishoni mwake:

﴿فَٱسۡتَجَابَ لَهُمۡ رَبُّهُمۡ﴾

“Basi Mola wako Mlezi akayakubali maombi yao[43]”.

---

[41]- Unapoomba usifanye haraka kujibiwa wala usikate tamaa, lakini endelea kukariri na kurejerejea dua yako, kwa sababu unapoomba dua Allaah anaweza kukujibu kwa haraka au akakufutia madhambi yako au akakuwekea malipo yako huko akhera ambako unahitajia zaidi msada wake.

[42]- Bukhari (6340) na Muslim (2735) na hili ni tamko la Muslim.

[43]- Surat Aal-Imraan (195).

Kwa hiyo inapasa kwa muislamu kutoharakisha kujibiwa, [kama alivyosema Ibnul Qayyim[44] -Allaah amrhemu-]:

«وَمِنَ الْآفَاتِ الَّتِي تَمْنَعُ تَرَتُّبَ أَثَرِ الدُّعَاءِ عَلَيْهِ: أَنْ يَسْتَعْجِلَ الْعَبْدُ، وَيَسْتَبْطِئَ الْإِجَابَةَ، فَيَسْتَحْسِرُ وَيَدَعُ الدُّعَاءَ، وَهُوَ بِمَنْزِلَةِ مَنْ بَذَرَ بَذْرًا أَوْ غَرَسَ غَرْسًا، فَجَعَلَ يَتَعَاهَدُهُ وَيَسْقِيْهِ، فَلَمَّا اسْتَبْطَأَ كَمَالَهُ وَإِدْرَاكَهُ تَرَكَهُ وَأَهْمَلَهُ»

“Miongoni mwa vizuizi ambavyo vinazuia kupatikana athari ya dua juu yake ni; mtu kuwa na haraka, na kuona kuchelewa kujibiwa, kisha anakata tamaa na kuacha kuomba dua, huyo ni sawa na yule ambaye amepanda mbegu, au ameotesha mmea, akawa anauhudumia na kuumwagilia, wakati alipoona kuchelewa kustawi kwake na kukua kwake aliuacha na kuupuuza[45]”.

na wala hakupata katika mmea huo kile alichokitaka. Na hapa Imam Ibnul Qayyim -Allaah amrehemu- ameitaja faida nzuri:

«وَأَلَحَّ عَلَيْهِ فِي الْمَسْأَلَةِ، وَتَمَلَّقَهُ»

“Akabembeleza juu yake katika maombi na akajipendekeza”.

Kubembeleza ni: kufanya upole katika maombi, anakusudia katika hili ya kwamba kubembeleza katika dua kunakuwa ni kwa upole na adabu, na kudhihirisha unyonge kwa Allaah na kuhitajia.

[44]- Mtunzi hakutaja maneno ya Ibnul Qayyim hapa lakini ameashiria kwa kutaja ukurasa tu, kwa hiyo nikaona si vibaya kuyahudhurisha hapa kama yalivyokuja katika asili yake.

[45]- Kitabu: [Al-Jawaabul Kaafi] (Uk. 15).

Jambo la Kumi

<<أَنْ يَجْمَعَ فِيْ دُعَائِهِ بَيْنَ الرَّغْبَةِ وَالرَّهْبَةِ>>

“Akusanye katika dua yake baina ya matumaini na khofu”.

Jambo la kukusanya baina ya matumaini na khofu lina umuhimu mkubwa katika dua na pia katika ibada nyingine, kwa sababu muislamu katika ibada zake anatakiwa awe na matumaini na khofu, na baina ya khofu na matarajio, kwa sababu hiyo wakati Allaah alipotaja visa vya Mitume katika suratul Anbiya', na namna alivyo waokoa na vitimbi na mitihani mbalimbali, akahitimisha kwa kusema:

﴿إِنَّهُمۡ كَانُواْ يُسَٰرِعُونَ فِي ٱلۡخَيۡرَٰتِ وَيَدۡعُونَنَا رَغَبٗا وَرَهَبٗاۖ وَكَانُواْ لَنَا خَٰشِعِينَ﴾

“Hakika wao walikuwa wepesi wa kutenda kheri, na wakituomba sisi kwa matumaini na khofu. Na walikuwa kwetu sisi ni wanyenyekevu[46]”.

Kwa hiyo walikusanya katika dua yao baina ya shauku na khofu, na maana ya **Raghba:** ni kuwa na matumaini na (kheri) zilizopo kwa Allaah, na **Rahba:** ni kuwa na khofu na machukivu yake, na uchungu wa adhabu yake.

[46]- Surat Al-Anbiyaa/90.

Na wakati Allaah alipotaja sifa za waumini waliokamilika akasema:

﴿وَٱلَّذِينَ يُؤْتُونَ مَآ ءَاتَواْ وَّقُلُوبُهُمْ وَجِلَةٌ أَنَّهُمْ إِلَىٰ رَبِّهِمْ رَٰجِعُونَ﴾

“Na wale ambao wanatoa walichopewa na hali ya kuwa nyoyo zao zinaogopa kwa kuwa watarejea kwa Mola wao Mlezi[47]”.

Wanajitahidi katika kufanya ibada kwa ajili ya kupata thawabu mbele za Allaah, pamoja na hivyo mioyo yao ina woga zisije kukataliwa amali zao, kwa hiyo wanakusanya katika ibada zao baina ya matumaini (ya kupata ujira mbele ya Allaah) na khofu (ya kutokubaliwa ibada zao hatimae Allaah akawaadhibu).

Na mfano wake ni dua ya Nabii Ibrahim -Alaihis salaam- wakati Allaah alipomuamrisha kujenga (Alka’ba), akaomba:

﴿رَبَّنَا تَقَبَّلْ مِنَّآ إِنَّكَ أَنتَ ٱلسَّمِيعُ ٱلْعَلِيمُ﴾

“Ewe Mola Mlezi wetu, Tutakabalie. Hakika wewe ni Msikizi Mjuzi[48]”.

[47]- Suratul Muuminiin/60.
[48]- Surat Al-Baqara/127.

(Aliomba dua hiyo) hali ya kuwa yeye ni miongoni mwa Mitume Ulul ‘azmi (Mitume wenye subra kubwa), na Allaah amemfanya kuwa ni khalili (mwandani wake), na amali yake anayoifanya ya kujenga nyumba ya Allaah Alka’ba ni katika amali iliyo tukufu mno, pamoja na hayo anamuomba Allaah amtakabalie yeye amali yake hiyo, ndio maana Wuhaib Bin Wardi -Allaah amrehemu- alipoisoma aya hii alilia na akasema:

«يَا خَلِيلَ الرَّحْمَنِ، تَرْفَعُ قَوَائِمَ بَيْتِ الرَّحْمَنِ وَأَنْتَ مُشْفِقٌ أَنْ لَا يَتَقَبَّلَ مِنْكَ»

“Ewe khalili (kipenzi) cha Allaah Mwingi wa rehma, unanyanyua jengo la nyumba ya Allaah mwingi wa rehma, na hali ya kuwa wewe ni mwenye kuogopa kwamba Allaah hatokukubalia![49]”.

[49]- Tafsiir Ibn Kathir (Jz. 1, Uk. 247).

Jambo la Kumi na Moja

<<التَّوَسُّلُ لِلَّهِ بِأَسْمَائه وَصِفَاتِهِ وَتَوْحِيْدِهِ>>

“Kujikurubisha kwa Allaah kwa majina, sifa na tauhidi yake”.

Kujikurubisha kwa Allaah kupitia majina yake, sifa na tauhidi yake ni katika sababu kubwa ya kujibiwa dua, na Allaah Subhaanahu wata’alaa ameamrisha (hilo) akasema:

﴿وَلِلَّهِ ٱلْأَسْمَآءُ ٱلْحُسْنَىٰ فَٱدْعُوهُ بِهَا﴾

“Na ana Allaah majina mazuri. Basi mwombeni kwayo[50]”.

Kwa sababu hii zimekuwa dua zote zilizopokewa kutoka kwa Mtume (Muhammad) -swala na salamu zimshukie- na Mitume wengine kabla yake -salamu ziwashukie- zimekusanya juu ya kujikurubisha kwa Allaah kwa majina na sifa zake, kama ilivyokuja katika dua ya Nabii wa Allaah Shuaib -salamu zimshukie-:

﴿رَبَّنَا ٱفْتَحْ بَيْنَنَا وَبَيْنَ قَوْمِنَا بِٱلْحَقِّ وَأَنتَ خَيْرُ ٱلْفَٰتِحِينَ﴾

“Ewe Mola wetu Mlezi, tuhukumie baina yetu na jamaa zetu kwa haki, nawe ndiye mbora wa wenye kuhukumu[51]”.

Na pia imekuja katika dua ya Nabii wa Allaah Issa -salamu zimshukie-:

[50]- Surat Al-A’raaf/180.
[51]- Surat Al-A’raaf/89.

﴿وَٱرۡزُقۡنَا وَأَنتَ خَيۡرُ ٱلرَّٰزِقِينَ﴾

“(Basi) turuzuku, na wewe ndiye mbora wa wanaoruzuku[52]”.

Na miongoni mwa dua ambazo Mtume -swala na salamu zimshukie- alimfunza Abubakar -Allaah amridhie- ni:

«اللَّهُمَّ إِنِّيْ ظَلَمْتُ نَفْسِيْ ظُلْمًا كَثِيرًا، وَلاَ يَغْفِرُ الذُّنُوبَ إِلَّا أَنْتَ، فَاغْفِرْلِيْ مَغْفِرَةً مِنْ عِنْدِكَ، وَارْحَمْنِيْ إِنَّكَ أَنْتَ الغَفُورُ الرَّحِيْمُ»

“Ewe Allaah, hakika mimi nimeidhulumu nafsi yangu dhulma kubwa, na wala hakuna anaesamehe madhambi isipokuwa wewe, basi nisamehe msamaha utokao kwako, na unirehemu, kwa sababu wewe ni Mwingi wa kusamehe Mwingi wa huruma[53]”.

Na Mtume -swala na salamu zimshukie- alikuwa anawafunza umma wake kujikurubisha kwake kupitia majina yake yote mazuri:

«مَا أَصَابَ أَحَدًا قَطُّ هَمٌّ وَلَا حَزَنٌ، فَقَالَ: اللهُمَّ إِنِّيْ عَبْدُكَ، ابْنُ عَبْدِكَ، ابْنُ أَمَتِكَ،نَاصِيَتِيْ بِيَدِكَ، مَاضٍ فِيَّ حُكْمُكَ، عَدْلٌ فِيَّ قَضَاؤُكَ، أَسْأَلُكَ بِكُلِّ اسْمٍ هُوَ لَكَ سَمَّيْتَ بِهِ نَفْسَكَ، أَوْ عَلَّمْتَهُ أَحَدًا مِنْ خَلْقِكَ، أَوْ أَنْزَلْتَهُ فِي كِتَابِكَ، أَوِ اسْتَأْثَرْتَ بِهِ فِي عِلْمِ الْغَيْبِ عِنْدَكَ، أَنْ تَجْعَلَ الْقُرْآنَ رَبِيعَ قَلْبِيْ، وَنُورَ صَدْرِيْ، وَجِلَاءَ حُزْنِيْ، وَذَهَابَ هَمِّيْ، إِلَّا أَذْهَبَ اللهُ هَمَّهُ وَحُزْنَهُ، وَأَبْدَلَهُ مَكَانَهُ فَرَحًا "، قَالَ: فَقِيلَ: يَا رَسُولَ اللهِ، أَلَا نَتَعَلَّمُهَا؟ فَقَالَ: " بَلَى، يَنْبَغِيْ لِمَنْ سَمِعَهَا أَنْ يَتَعَلَّمَهَا»

[52]- Surat Al-Maida/114.
[53]- Bukhari (834) na Muslim (2705).

“Haijamsibu mtu yeyote huzuni wala hamumi (jekejeke la roho) kisha: akasema: Ewe Allaah mimi ni mja wako, mtoto wa mja wako, mtoto wa mjakazi wako, utosi wangu uko mikononi mwako, ni yenye kupita kwangu hukumu yako, na ni ya uadilifu kwangu Qadari yako, ninakuomba kwa kila jina ambalo ni lako, umejiita kwalo kwenye nafsi yako, au umeliteremsha ndani ya vitabu vyako, au umejihusisha nalo katika elimu ya ghaibu iliyopo kwako, uijaalie Qur’an tukufu ni yenye kukuza moyo wangu, na ni nuru ya kifua changu, na yenye kuondosha huzuni na hamumi yangu, isipokuwa Allaah atamuondoshea huzuni yake, na atabadilisha mahala pake kuwa ni faraja”. Ikasemwa: Ewe Mtume wa Allaah, je tusijifunze? Akasema: “kwanini! Inapasa yule aliyesikia ajifunze (dua hiyo)[54]”.

Na aliposema Imam Ibnul Qayyim -Allaah amrehemu-: “وَتَوْحِيْدِهِ” anakusudia kwamba, inapasa kutawasali/kujikurubisha kwa Allaah kupitia sababu hizi kubwa, ambazo ni kumpwekesha Allaah (Tauhid) na kumuamini yeye.

Na miongoni mwa ushahidi wa kutawasali na vitu hivyo ni kile alichotaja Allaah katika dua za waumini:

[54]- Kitabu: [Musnad Ahmad] (3712). Na ameisahihisha sheikh Albani katika [As silsila] namba: (199).

﴿رَبَّنَآ إِنَّنَا سَمِعۡنَا مُنَادِيٗا يُنَادِي لِلۡإِيمَٰنِ أَنۡ ءَامِنُواْ بِرَبِّكُمۡ فَـَٔامَنَّاۚ رَبَّنَا فَٱغۡفِرۡ لَنَا ذُنُوبَنَا وَكَفِّرۡ عَنَّا سَيِّـَٔاتِنَا وَتَوَفَّنَا مَعَ ٱلۡأَبۡرَارِ﴾

“Ewe Mola wetu Mlezi, hakika sisi tumemsikia mwenye kuita akiita kwenye Imani kwamba: Muaminini Mola wenu Mlezi, nasi tukaamini. Ewe Mola wetu, basi tusamehe madhambi yetu na utufutie makosa yetu, na utufishe pamoja na watu wema[55]”.

Na wakati Mtume -swala na salamu zimshukie- alipomsikia mtu mmoja anaomba dua akisema:

"اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ أَنِّيْ أَشْهَدُ أَنَّكَ أَنْتَ اللَّهُ، لَا إِلَهَ إِلَّا أَنْتَ، الْأَحَدُ الصَّمَدُ الَّذِيْ لَمْ يَلِدْ، وَلَمْ يُولَدْ، وَلَمْ يَكُنْ لَهُ كُفُوًا أَحَدٌ"، فَقَالَ: «لَقَدْ سَأَلْتَ اللَّهَ بِالِاسْمِ الَّذِيْ إِذَا سُئِلَ بِهِ أَعْطَى، وَإِذَا دُعِيَ بِهِ أَجَابَ»

[Ewe Allaah hakika mimi ninakuomba (wewe kheri kwa kutawasali na kukusifu) kwa sababu mimi ninashuhudia kwamba wewe ni Allaah, hapana wa kuabudiwa kwa haki ila wewe, Uliye mmoja Mwenye kukusudiwa katika haja zote ambaye hakuzaa wala hakuzaliwa, wala hakuna kitu chochote ni mfano kwake yeye]. Akasema: **“Kwa hakika umemuomba Allaah kwa jina ambalo akiombwa (chochote) kwalo anatoa, na akiombwa dua kwalo anajibu[56]”.**

[55]- Surat Aal Imraan/193.
[56]- Sunan Abi Daud (1493), na ameisahihisha sheikh Albani.

Jambo la Kumi na Mbili:

<<التَّصَدُّقُ بَيْنَ يَدَيِ الدُّعَاءِ>>

“Kutanguliza kutoa sadaka kabla ya dua”.

Sadaka ina athari kubwa, kama imethibiti kutoka kwa Mtume -swala na salamu zimshukie- kwamba yeye amesema:

«وَصَدَقَةُ السِّرِّ تُطْفِئُ غَضَبَ الرَّبِّ»

“Na sadaka ya siri inazima machukivu ya Mola Mlezi[57]”.

Hapana shaka kwamba Allaah kuondosha machukivu yake kwa mja ni sababu ya kujibiwa dua yake na kumpa yeye kile anachokiomba.

Na huko (kutoa sadaka) ni miongoni mwa amali njema ambazo ameruhusiwa muislamu kutawasali/kujikurubisha kwazo katika kumuomba Allaah.

[57]- Kitabu: [Mu’jamul Kabiir] ya imamu At-Twabraani] (8014), na ameisahihisha sheikh Albani.

Jambo la Kumi na Tatu:

<<تَحَرِّي الأَدْعِيَةِ الَّتِيْ أَخْبَرَ النَّبِيُّ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ أَنَّ الدُّعَاءَ مَعَهَا مُسْتَجَابٌ>>

“Kufanya pupa (katika) kuomba dua ambazo ameeleza Mtume -swala na salamu zimshukie- kwamba dua ni yenye kujibiwa kwa haraka (ikiombwa) pamoja na dua hizo”.

Endapo muislamu atafanya pupa ya kuomba dua hizi ambazo zimethibiti, tena akaziomba (dua) hizo kwa ukweli, kubembeleza pamoja na kuhudhurisha mambo yote yaliyotangulia, basi hakika dua yake haikurubii kabisa kukataliwa.

Na mfano wa dua hizo ni kauli ya Mtume -swala na salamu zimshukie-:

«دَعْوَةُ ذِي النُّونِ إِذْ دَعَا وَهُوَ فِي بَطْنِ الحُوتِ: لاَ إِلَهَ إِلاَّ أَنْتَ سُبْحَانَكَ إِنِّي كُنْتُ مِنَ الظَّالِمِينَ، فَإِنَّهُ لَمْ يَدْعُ بِهَا رَجُلٌ مُسْلِمٌ فِي شَيْءٍ قَطُّ إِلاَّ اسْتَجَابَ اللَّهُ لَهُ».

[Dua ya Dhin-Nun (Nabii Yunus) wakati alipoomba hali ya kuwa yumo tumboni mwa Chewa, (alisema):

﴿لَّآ إِلَٰهَ إِلَّآ أَنتَ سُبْحَٰنَكَ إِنِّي كُنتُ مِنَ ٱلظَّٰلِمِينَ﴾

“Hapana Muabudiwa (wa haki) isipokuwa wewe, kutakasika na makosa ni kwako. Hakika nilikuwa miongoni mwa wenye kudhulumu”. Hakika hataomba kwa dua hiyo mtu yeyote

muislamu katika dhiki yoyote isipokuwa Allaah atamuitikia[58].

Na imepokewa kutoka kwa Anas Bin Malik -Allaah amridhie-, kwamba Mtume -swala na salamu zimshukie- alimsikia mtu mmoja[59] akisema katika dua yake:

"اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ بِأَنَّ لَكَ الْحَمْدُ، لَا إِلَهَ إِلَّا أَنْتَ الْمَنَّانُ، بَدِيعُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ، يَا ذَا الْجَلَالِ وَالْإِكْرَامِ، يَا حَيُّ يَا قَيُّومُ"، فَقَالَ النَّبِيُّ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ: «لَقَدْ دَعَا اللَّهَ بِاسْمِهِ الْعَظِيمِ، الَّذِي إِذَا دُعِيَ بِهِ أَجَابَ، وَإِذَا سُئِلَ بِهِ أَعْطَى»

[Ewe Allaah hakika mimi ninakuomba wewe (kheri kwa kutawasali na kukusifu wewe), kwa sababu ni zako wewe tu sifa njema zote, Hapana Muabudiwa (wa haki) isipokuwa wewe, Mwenye kipawa (mwenye kutoa), muumba wa mbingu na ardhi, ewe mwenye utukufu na ukarimu, ewe uliye hai mwenye kusimamia kila kitu]. Akasema Mtume -swala na salamu zimshukie-: **"Kwa hakika amemuomba Allaah kwa jina tukufu, ambalo akiombwa kwalo anajibu, na akiombewa kwalo (kitu chochote) anatoa[60]".**

Haya ni jumla ya masharti na adabu katika kuomba dua ambazo amezitaja Imam Ibnul Qayyim -Allaah amrehemu-, basi inapasa

[58]- Tirmidh (3505) na Ahmad (1462). Ameisahihisha sheikh Albani katika sahihi Tirmidh (2785).
[59]- Anaitwa Abu 'Ayaash Zaid Bin Swaamit Az-Zuraqi.
[60]- Sunan Abi Daud (1495) na ameisahihisha sheikh Albani.

kwa kila muislamu ajitahidi kuzipatiliza katika dua zake, kwa sababu wakati wowote yakikusanyika (hayo) ni kama alivyosema Ibnul Qayyim (Allaah amrehemu) :

"فَإِنَّ هَذَا الدُّعَاءَ لَا يَكَادُ يُرَدُّ أَبَدًا"

“Hakika dua (ya namna) hii haikurubii kabisa kukataliwa”.

Tunamuomba Allaah Ta’alaa atutengenezee Dini yetu ambayo ndio kinga ya mambo yetu, na atutengenezee Dunia yetu ambayo humo kuna maisha yetu, na atutengenezee akhera yetu ambayo ndio marejeo yetu, na ajaalie uhai (wetu) ni kwa ajili ya kuzidisha kheri, na ajaalie kifo (chetu) ni raha kwetu na kila shari.

Na Allaah ndiye Mjuzi zaidi.

Swala na Salamu Zimshukie Mtume wetu Muhammad, Jamaa zake na Maswahaba wote[61].

Abu Halima Arafat Bin Mahmoud,

Imekamilika siku ya Ijumaa,

16/Shawwaal/1442h -10/5/2021m,

Pongwe Tanga/Tanzania.

[61]- Amesema Sheikh Abdul Razzaq -Allaah amhifadhi-: “Asili ya Risala hii ni Muhadhara uliotolewa huko mji wa Madina katika Majlis Ibrahim Al-Waqiis -Allaah amrehemu-, siku ya juma tatu 24/6/1441H, baadhi ya ndugu wakaiweka katika maandishi na kuichapisha, na mimi nikaipitia na kuisahihisha, na nikazidisha ndani yake baadhi ya mambo na faida mbalimbali. Namuomba Allaah amlipe kheri kila aliyeshiriki kuitoa kazi hii, kuineza na kuisambaza kwa waislamu (Aamin).